Kuja Kwa Yesu Mara Ya Pili

“Kuja kwa kristo mara ya pili ndilo tumaini lenye baraka la kanisa, hitimisho kuu la injili. Kuja kwa mwokozi kutakuwa halisi, binafsi, kutaonekana kwa dunia mzima. Atakaporudi wenye haki waliokufa watafufuliwa na pamoja na wenye haki walio hai watavikwa utukufu na kuchukuliwa kwenda mbinguni, lakini waovu watakufa. Kutimizwa karibu kabisa kwa sehemu nyingi za unabii, pamoja na hakli ya sasa ya ulimwengu, huonyeshe kwamba kuja kwa kristo ku karibu sana. Wakati wa tukio hilo hakukufunuliwa, na hivyo basi tunahimizwa kuwa tayari kwa nyakati zote.” (Tit.2:13, Mt. 24; Mdo1: 9-11, Mt.24:14; Ufu. 1:7, 14:14-20; Mt. 24:43-43, 1Kor.15:51-50, 1Thes1:7, 4:13-18, 5:1-6, Mk 13; Luk 21:2; 2Tim 3:1-5).

Mama, mtoto moja alisema kabla ya kulala, akimwambia mama yake, natamani sana kuonana na rafiki yangu Yesu. Je, atakuja lini? Mtoto huyu mdogo alikuwa hajui kwamba tamanio lake la kurudi kwa Yesu ni tamanio la dahari (enzi). Maneno ya mwisho kwenye Biblia hutoa ahadi ya kuja kwa Yesu “Naam naja upesi” na mtume Yohana anaongeza “Amina, naam na uje Bwana Yesu.” Uf. 22:20. Kumwona Yesu!!! Kuungana milele na atupendaye kuliko tunavyoweza kufikiri! Kukomesha maumivu, vilio magonjwa na mauti, kufurahia umilele pamoja na watakatifu waliofufuliwa ambao kwa sasa wanapumzika makaburini! Ni tumaini lenye kuburudisha kwa kiasi gani!

Maelezo ya kuja kwa Yesu

Naam, siku moja Yesu atakuja. Kuja kwake litakuwa ni jambo la kushangaza kwa waliosubiri kwa muda mrefu hata wakalala usingizi (Mt. 25:5). Usiku wa manane, (Mt. 25:6) ikimaanisha wakati dunia ikiwa katika enzi za giza nene, Mungu atadhihirisha uwezo kuokoa watu wake. Maandiko hutoa maelezo ya kuja kwa Yesu: Sauti kubwa itatoka kwenye Hekalu, kwenye kiti cha enzi ikisema Imekwisha kuwa (Ufu. 16:17), patakuwa na umeme, sauti ya radi, tetemeko kubwa juu ya nchi, (Uf. 16:18), milima itatetemeka, miamba itavunjika vunjika na kutawanyika kama mawimbi ya bahari, miji itaanguka, visiwa vitakimbia (Uf. 16:20). Mbingu zitakunjwa kama ukurasa, milima na visiwa vitaondolewa mahali pake (Uf. 6:14).

Pamoja na vurugu ya maumbile ya nchi, watu wa Mungu watakuwa na ujasiri kwa kuwa wataiona ishara ya kuja kwake Mwana wa Adam (Mt. 25:30). Atakapokuwa anashuka na mawingu (Mdo. 1:9-11), kila jicho litamwona (Uf. 1:7), akiwa Mfalme wa uzima na siyo mtu wa sikitiko, siyo aliyevaa taji ya miiba bali amevaa taji ya utukufu, (Uf. 19:12) na jina lililoandikwa kwenye vazi lake na paja lake MFALME WA WAFALME NA BWANA WA MABWANA (Uf. 19:16).

Atakapokuwa anakuja, hofu itawakumba wote waliokataa neema yake pale alipowasihi “ghairini, muachane na njia yenu mbaya, mbona mnataka kufa?” (Ez. 33:11.). Wafalme, wakuu, majemedari, matajiri, wenye nguvu, kila mtumwa na mwungana watajificha chini ya miamba na milima wakiiambia milima na miamba tuangukieni, tusitirini mbele za uso wake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi na hasira za Mwanakondoo (Uf. 6:15, 16). Kwa maana siku ya hasira yake imekuja naye ni nani awezaye kusimama? (Uf. 6:17). Furaha yao waliomtazamia kurudi itafunika hofu ya waovu. Kuja kwa mkombozi inahitimisha historia ya watu wa Mungu kwa utukufu. Kwa sauti yenye kupenya watasikika wakisema “Tazama huyu ndiye Mungu wetu, ndiye tuliyemngoja atusaidie. Huyu ndiye BWANA tuliyemngoja, na tushangilie na kuufurahia wokovu wake” (Isa. 25:9).

Atakapokaribia, atatuma sauti kubwa ya parapanda kuwakusanya wateule wake toka pande zote za dunia (Mt. 24:31). Ni kipindi cha kufurahisha kwa kuwa watakatifu walioko makaburini wataisikia sauti yake! (Yoh.5:28). Wale watakatifu watakaokutwa hai kufumba na kufumbua watabadilika (1Kor.15:52). Wakiwa wamevikwa utukufu na kutokufa, pamoja na watakatifu waliofufuliwa, watanyakuliwa kumlaki BWANA angani na kuwa naye milele (IThes. 4:16, 17).

Mafundisho ya kuzingatia kuhusiana Yesu kuja mara ya pili

Uhakika wa Kuja kwake

Mitume na wakristo wa awali waliokuona kuja kwa Yesu kuwa tumaini lenye Baraka (Tit. 2:13 cf Ebr. 9:28). Walitumainia unabii na ahadi zote za Maandiko Matakatifu vitatimia wakati wa Yesu kuja mara ya pili. (2 Pet. 3:13 cf Isa. 65:17) kwa kuwa hilo ndilo lengo la safari ya kikristo. Wote wanaompenda Kristo wanatazamia fursa watakayomwona Yesu na kuwa na ushirika na Baba pamoja na Roho Mtakatifu.

Ushahidi wa Biblia kuwa Yesu anakuja tena

Yoh. 14: 3 Nami nikienda nitarudi tena niwakaribishe kwangu ili nilipo nanyi mwepo

Henoko alitabiri juu ya kuja kwa Yesu akiwa na utukufu Yuda 14, 15.

Miaka 1,000 kabla Yesu hajazaliwa, mtunga zaburi alitabiri atakuja na hatanyamaza... na kuwaita wale waliofanya naye agano kwa dhabihu (Zab. 50: 3 - 5)

Siku Yesu aliyopaa, malaika walitoa ahadi kwamba atarudi kama alivyoondoka Mdo. 1: 9 – 11

Garantii (Amana) ya Yesu kuja mara ya pili ni kuja kwake mara ya Kwanza

Mara ya kwanza Yesu alikuja kuokoa, mara ya pili anakuja kukamilisha kile alichokiokoa kwa kukivika utukufu. Yesu alikuja akapata ushindi usiohojiwa (Wafil. 2:15) na hivyo ni muhimu akaja kukamilisha wokovu (Ebr. 9:26, 28).

Huduma ya Kristo inayoendelea Mbinguni

Ufunuo kwa Yohana unadhihirisha kwamba hekalu la mbinguni ni jambo la msingi kwa ajili ya mpango wa Mungu wa wokovu. (Uf. 1:12, 13, 3:12, 4:1-5, 5:8, 7:15, 8:3, 11:1, 19, 14:15, 17; 15:5, 6, 8; 16: 1, 17). Unabii unaosema kwamba ameanza huduma ya mwisho kwa mwenye dhambi, huongeza kwamba atarudi kuwachukua watu wake. (Ebr. 9:26, 28 cf Uf. 15:8, Uf. 16:15)

Namna atakavyokuja

Yesu alionya kwamba watatokea waongo ambao watapotosha juu ya ujio wake, wakisema ameonekana huku au kule na akaonya tusiwaamini (Mt. 24, 24, 23). Sasa anakuja vipi?

Atakuja kama alivyoondoka, Mdo. 1: 9- 11, akiwa na mwili bila kuwa katika roho Luk. 24: 36 – 43

Kuja kwake kutaonekana. Kama umeme toka mashariki hadi magharibi (Mt. 24: 27), Wanadamu watamwona (Uf. 1: 7) na kutakuwa na nafasi ya kuomboleza (Mt. 24:30).

Kuja kwake kutasikika: Kutaambatana na mlio wa baragumu (1Thes. 4:13, Mt. 24:31)

Atakuja na utukufu wa Baba yake (Mt. 16:27, Uf. 19:11-16)

Kama siku za Babeli, ufalme wa Mungu hautasimama pamoja na falme zingine Dan. 2: 34, 44, 35)

Kuja kwa Yesu na matokeo yake kwa wanadamu

Atawakusanya watakatifu (Mt. 24:31, Mt. 25:34, 35; Mk. 13:27), na kuwapa kuishi naye (Yoh. 14:3) Atawafufua watakatifu waliokufa Katika Kristo 1 Kor. 15:52, 53, 1 Thes. 4:16). Watakatifu wataizomea mauti (1Kor. 15: 55), nao watavikwa utukufu wakiakisi utukufu wa Mungu katika miili, akili na roho (1Kor. 15: 42-54) Waovu wataangamizwa (2 Thes. 2:9 -12, Uf. 6: 16, 17) kwa upanga utokao kutoka kwake yeye aketiye juu ya farasi (Uf. 19:20, 21).

Dalili za Kuja kwa Yesu mara ya Pili

Biblia haifundishi tu jinsi Yesu atakavyokuja mara ya pili bali pia imesema dalili za kuja kwake. Hapa tunaziangalia kwa ujumla na kwa ufupi.

Dalili juu ya ulimwengu wa asili. Dalili juu ya jua kutiwa giza, mwezi kutokutoa nuru na nyota kuanguka (Luk. 21:25, Mk. 13:24-26). Yohana aliona tetemeko kubwa (Uf. 6:12). Hizi dalili zilionyesha kukoma kwa miaka 1260 za Uf. 12:6)

Dalili juu ya ulimwengu wa kidini. Kuwepo uamsho mkubwa (Uf. 14:6,7). Kitabu cha Danieli kitafunguliwa (Dan. 12:4) na kuhubiriwa kwa ujumbe wa malaika watatu (Uf. 14: 6-12) Kuhubiriwa injili Mt. 24:14, na watu wa Mungu kuitazamia siku ya kuja kwake (2 Pet. 3:12) Kupoa kwa hali ya kiroho (Mt. 24:12, 2Tim. 3: 1-5) Kuibuka Upapa (Uf. 13:3,) nabii wa uwongo (Uf. 16:13, 14), Mnyama (Uf. 16: 13, Uf. 3:13) Kupungua kwa uhuru wa kuabudu (Uf. 13: 17, 15; Uf. 14: 9-12) Taabu kwa watakatifu (Dan. 12:1)

Kuongezeka Uovu. Kwa kuwa limezuka fundisho kwamba kutii amri za Mungu siyo jambo muhimu, dunia inaendelea kujaa maovu ya kila aina. Kama ilivyokuwa siku za Nuhu, (Mt.
24:37-39), maovu ya zinaa (Mw. 6:2) dhuluma (Mw. 6:11, Yak. 5: 1-6)

Vita na Majanga. Taifa litaondoka kupigana na taifa, ufalme kupigana na ufalme, kutakuwa na njaa... (21:10, 11; Mk. 13:7, 8; Mt. 24: 7)

Kuwa tayari wakati wote

Biblia hutufundisha kwamba Yesu anakuja lakini haijatuambia anakuja lini (Mt. 24:36). Matayarisho ya Mkristo yanapaswa kuwa ya siku zote ili tusije kukataliwa na Mungu (Mt. 7:21 -24). Mfano wa wanawali 10 huonyesha wako wakristo watakaokuja kukataliwa (Mt. 25:11, 12).

Kabla ya gharika Mungu alimtuma Nuhu (Mw. 6:13), kabla ya kuiharibu Sodoma alituma Malaika (Mw. 19) na kabla ya Yesu atatuma ujumbe “Heri aliyealikwa kwenye arusi ya mwana kondooo Uf. 19:9). Watakaosikia sauti ya Mungu ndio watakaoshangilia kuja kwake (Isa. 25: 9)